WIZARA YA NISHATI

# News Bulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 65 | Aprili 1 - 30 2025



# TIJA KWA NCHI NDIYO KIPAUMBELE CHA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA (LNG) - DKT.BITEKO

WIZARA YA NISHATI +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**

Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika

**WAPIGA PICHA**

Henry Kilasila
Godfrey Mwemz
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo
Mustafa Shahame

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga


© NISHATI 2025

# TIJA KWA NCHI NDIYO KIPAUMBELE CHA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA (LNG)- DKT.BITEKO



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt.Doto Biteko, akijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati ya shilingi Trilioni 2.2 kwa mwaka 2025/2026 kabla ya kupitishwa kwa kishindo na Bunge hilo kwa asilimia 100, 29 Aprili 2025 bungeni jijini Dodoma

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt.Doto Biteko amesema dhamira ya Serikali ni kutekeleza mradi mkubwa wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG) kutokana na faida zake kiuchumi ila kwa sasa kuna maeneo ambayo Serikali inayafanyia kazi kwa kina kupitia majadiliano na Wawekezaji ili mradi husika uwe na tija kwa nchi na wananchi.

Ameyasema hayo tarehe 29 Aprili 2025 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati ya shilingi Trilioni 2.2 kwa mwaka 2025/2026 kabla ya kupitishwa kwa kishindo na Bunge hilo kwa asilimia 100. " Mradi wa LNG umeanza kusemwa kwa muda mrefu na kila mmoja angetamani mradi huu ukamilike jana lakini lazima tukubaliane kuwa lazima tujadiliane kwa kina na wawekezaji ili kupata kilicho bora na kuleta tija, ninachotaka kuwahakikishia ni kuwa timu ya majadiliano ya Serikali na Wawekezaji wanaendelea na majadiliano na tunatarajia kuwa ndani ya mwaka huu 2025 kama tutakuwa tumemaliza masuala matatu yaliyosalia kujadiliwa, mkataba huo utasainiwa ili mradi uanze mara moja." Amesema Dkt.Biteko

Ameongeza kuwa, Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ana kiu ya kuona mradi huo unaanza na alishatoa maagizo kwa Wizara ya kuhakikisha kuwa mradi unaanza kutekelezwa.

Akijibu hoja kuhusu vituo vya mafuta vinavyoongezeka na kujengwa kwa kukaribiana, Dkt.Biteko amesema kuwa Wizara ya Nishati imeanza mazungumzo na Wizara ya Ardhi ili kuongeza umbali kati ya kituo kimoja na kingine kutoka mita 200 za sasa kwa lengo la kuleta usalama wa watu, mazingira na shughuli za kijamii.

Kuhusu msamaha wa kodi mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa gesi inayotumika kwenye vyombo vya moto kama vile magari (CNG), Dkt. Biteko amesema kuwa Serikali ilishatoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa vifaa na mashine mbalimbali zinazotumika katika mnyororo wa thamani kwa miradi ya CNG kama vile mitungi ya CNG pamoja na vifaa vya kuwezesha kufunga mfumo kuwezesha magari kutumia gesi hiyo.

Ameongeza kuwa, katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Nishati

imewasilisha Wizara ya Fedha mapendekezo ya maboresho ya kodi katika gesi asilia inayotumika kwenye magari ili kuzidi kuhamasisha matumizi ya CNG na wawekezaji wanaowekeza kwenye miradi hiyo wapate faida na kurudisha gharama wanazowekeza kwa haraka.

Akijibu hoja za Wabunge kuhusu gharama za kuunganisha umeme vijijini na mijini, Dkt. Biteko amesema kuwa imeundwa timu kwa ajili ya kuangalia namna gani gharama hizo zitapunguzwa lengo likiwa ni kuleta unafuu kwa wananchi. Kuhusu usambazaji wa umeme Vijijini, Dkt.Biteko amesema kuwa, Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan anapaswa kupongezwa kwa kufikisha umeme katika Vijiji vyote 12,318 kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 huku kazi ya kupeleka umeme vitongojini ikiendelea kwa kasi.

Akizungumzia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika wilaya zote nchini kupitia mradi wa gridi imara, Dkt. Biteko amesema kuwa tayari Serikali imeshanunua viwanja kwa ajili kujenga vituo hivyo na katika awamu ya kwanza vitajengwa vituo 14 huku utekelezaji ukiendelea na katika laini za umeme ambazo ni ndefu sana Serikali itaweka switching stations.

Aidha, kuhusu suala la kukatika kwa umeme nchini, Dkt.Biteko amesema kuwa limepungua kwa asilimia 48 huku dakika za kukatika umeme zikipungua kwa asilimia 64 na kwa sasa umeme ukikatika ni kwa sababu tu ya matengenezo ya miundombinu. Hata hivyo amesema Serikali inaendelea kuimarisha kituo cha huduma kwa Wateja TANESCO ili taarifa ziwafikie wananchi kwa wakati pale umeme unapokatika ikiwemo kila wilaya kuwa na kundi sogozi.

Awali, wakati wa kuhitimisha Hotuba hiyo ya Wizara ya Nishati, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga alimpongeza Rais, Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya katika Taifa hususan kwenye Sekta ya Nishati akieleza kuwa moja ya misingi ya ukuaji wa kiuchumi na



maendeleo katika Taifa lolote ni uwekezaji katika Sekta ya Nishati.

Akizungumzia mikoa ambayo bado haijaunganishwa katika gridi ya Taifa ya umeme, Kapinga alisema kuwa kuna miradi mbalimbali inayoendelea ambapo katika Mkoa wa Rukwa kuna mradi mkubwa wa kusafirisha umeme unaoendelea wa kutoka Iringa-Tunduma hadi Rukwa na kipande kingine cha mradi kitakachounganisha gridi ya Tanzania na Zambia. "Mhe.Spika katika Mkoa wa Mtwara na Lindi tayari mkandarasi yupo eneo la kazi, mradi umeanza kwa kujenga njia ya umeme kutokea Songea-Tunduru-Masasi hadi Mahumbika na tumeshaanza kulipa fidia katika eneo la Tunduru hadi Masasi takriban shilingi bilioni 4.6 na eneo lililobakia la Songea kuelekea Namtumbo na Tunduru tutaendelea kulipa fidia ya takriban shilingi bilioni 2.7." Alisema Kapinga

Kuhusu kupeleka gridi ya Taifa katika Mkoa wa Kagera alisema kuwa kazi inaendelea kupitia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Benaco-Kyaka na katika Mkoa wa Katavi mradi wa kupeleka umeme wa gridi mkoani humo uko katika hatua za mwisho.

Akizungumzia kazi ya kupeleka umeme kwenye visiwa mbalimbali nchini, Kapinga alisema kuwa, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 9.89 ili kupeleka mifumo ya umeme jua katika visiwa 118 ambavyo vipo katika mikoa zaidi ya mitano hususan Wilaya ya Ukerewe.

Kuhusu maboresho miundombinu ya umeme katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Kapinga alieleza kuwa kuna kazi zinaendelea kwa lengo la kuwawezesha wananchi kupata umeme wa uhakika ikiwemo uboreshaji wa kituo cha Mbagala ambacho kilikuwa na transfoma yenye uwezo wa MVA 50 lakini sasa inawekwa transfoma mpya yenye uwezo wa MVA 120 ili kukiongezea uwezo kituo hicho ili wananchi wa Mbagala, Temeke, Yombo, Mkuranga na baadhi ya maeneo ya Kigamboni waendelee kupata umeme wa uhakika. Alieleza kuwa kazi hiyo imefikia mwishoni na muda wowote transfoma hiyo itaanza kufanya kazi. Kwa eneo la Kigamboni amesema maboresho pia yanaendelea kufanyika na kwamba wananchi tayari wameshaanza kuona mabadiliko ya upatikanaji umeme kupitia maboresho hayo.

# DKT.BITEKO AWASILISHA BUNGENI BAJETI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2025/2026

- Yagusa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa asilimia 96.5
- Upatikanaji umeme wa uhakika, Nishati Safi ya Kupikia, Uendelezaji Gesi Asilia; Ni baadhi ya vipaumbele vya Bajeti
- Kukamilika kwa JNHPP, Usambazaji Umeme Vijijini na Ufikishaji Gridi Kigoma; Ni baadhi ya mafanikio makubwa bajeti 2024/2025
- Kamati ya Bunge yaridhishwa na utekelezaji wa Bajeti ya Wizara 2024/2025

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameliomba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/2026 ya kiasi cha shilingi Trilioni 2.2 ambapo asilimia 96.5 ya Bajeti yote ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na asilimia 3.5 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Akiwasilisha Bajeti hiyo tarehe 28 Aprili, 2025 bungeni jijini Dodoma, Dkt.Biteko ametaja vipaumbele mbalimbali vya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/2026 ikiwemo kuendelea kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, pamoja na kufikisha Gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara.

" Mhe. Spika, kipaumbele kingine ni kuendelea na usambazaji wa nishati katika vitongoji, maeneo ya migodi, kilimo, viwanda na pampu za maji pamoja na vituo vya afya ili kuwezesha shughuli za uzalishaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi." Ameeleza Dkt.Biteko

Ametaja kipaumbele kingine kuwa ni upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa na kufanya matengenezo na ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme.

Pia kuhamasisha na kuwezesha watanzania kutumia nishati safi



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt.Doto Biteko akisoma bajeti ya Wizara ambapo ameliomba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuidhinisha Bajeti kwa mwaka 2025/2026 ya kiasi cha shilingi Trilioni 2.2 ambapo asilimia 96.5 ya Bajeti ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na asilimia 3.5 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Jijini Dodoma tarehe 28 Aprili 2025

ya kupikia ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034) na Mpango wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 – 2030.

Dkt. Biteko ametaja kipaumbele kingine kuwa ni kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa na kufanya matengenezo na ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme.

Pia, kuendelea kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za mafuta vijijini kupitia ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo.

Dkt. Biteko ameongeza kuwa kipaumbele kingine cha Bajeti ya 2025/2026 ni kutekeleza shughuli za utafutaji, uendelezaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia na kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia.

Vilevile kusimamia na kuhakikisha nchi inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja kuimarisha matumizi ya gesi asilia (CNG) katika vyombo vya moto.

Ameongeza kuwa kipaumbele kingine ni kuendelea kutekeleza shughuli za kiudhibiti kwa kuimarisha ushiriki wa wazawa katika Sekta ya Nishati pamoja na kuimarisha nguvu kazi na kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi ili kuimarisha tija na ufanisi katika utendaji kazi.

Pia kuongeza mchango wa nisha-

ti jadidifu katika uzalishaji wa umeme na ushiriki wa Sekta Binafsi katika maendeleo ya Sekta ya Nishati na kuanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 - 2030 (National Energy Compact 2025 - 2030) kuhusu upatikanaji na uunganishaji wa umeme kwa wananchi.

Awali Dkt.Biteko alilieleza Bunge la Tanzania kuhusu mafanikio mbalimbali ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ikiwemo kukamilika kwa mradi wa kielelezo wa kuzalisha umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115 na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 160 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Chalinze mkoani Pwani.

Ametaja mafanikio mengine kuwa ni kukamilika kwa Ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Chalinze na kuingiza umeme unaozalishwa JNHPP kwenye Gridi ya Taifa pamoja na kukamilika kwa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida hadi Arusha.

Mafanikio mengine yaliyopatikana katika Bajeti ya 2024/2025 ni kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa kutoka MW 1,601.84 Mwaka 2020/21 hadi MW 4,031.71 na kukamilika kwa Ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Chalinze na kuingiza umeme unaozalishwa JNHPP kwenye Gridi ya Taifa.

Pia kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma na kuunganisha Mkoa wa Kigoma kwenye Gridi ya Taifa na kufanikiwa kuokoa kiasi cha Shilingi bilioni 58.4 zilizokuwa zinatumika kwa mwaka kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya dizeli katika mkoa wa Kigoma.

Katika usambazaji wa umeme vijijini, Dkt. Biteko amesema kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imefikisha miradi ya umeme katika vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara kutoka vijiji 506 vilivyokuwa vimeunganishiwa umeme mwaka 2007 wakati REA inaanzishwa. Pia, kufikisha umeme kwenye vitongoji 33,657 kati ya 64,359 sawa na asilimia 52.

Dkt. Biteko ametaja mafanikio mengine kuwa ni kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 115 kutoka Tabora hadi Urambo na hivyo kuimarisha upatikanaji wa umeme Urambo pamoja na kuongezeka kwa uhamasishaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwemo usambazaji wa mitungi ya gesi ya kupikia 266,000 na majiko banifu 5,000 kwa wananchi.

Mafanikio mengine ya Bajeti ya 2024/2025 ni kuimarika kwa upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara kutokana na kufungwa kwa mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa MW 20 katika eneo la Hiyari – Mtwara pamoja na kuongezeka kwa wateja waliounganishiwa umeme nchini kutoka 2,766,745 Mwaka 2020/21 hadi 5,449,278 mwezi Aprili, 2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 97.

Katika Sekta ndogo ya Gesi Asilia, Dkt. Biteko amesema kuwa kumekuwa na ongezeko la mtandao wa usambazaji wa gesi asilia nchini kutoka kilomita 102.54 Mwaka 2020/21 hadi kilomita 241.58 mwezi Aprili 2025 ambao umewezesha kuunganishwa kwa jumla ya nyumba 1,514, taasisi 13 na viwanda 57.

Vilevile kumekuwa na ongezeko la ushiriki wa TPDC katika Kitalu cha uzalishaji wa gesi asilia cha Mnazi Bay kutoka asilimia 20 hadi asilimia 40 na kutolewa Leseni ya Uendelezaji wa Kitalu cha kuzalisha gesi asilia cha Ntorya kwa TPDC ambayo itashirikiana na Kampuni ya ARA Petroleum katika uendelezaji wa kitalu hicho.

Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa vituo vya kujaza gesi asilia (CNG filling stations) kwenye vyombo vya moto kutoka vituo viwili (2) Mwaka 2020/21 hadi vituo tisa (9) mwezi Aprili 2025 pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania katika shughuli za utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia hadi asilimia 90 ikilinganishwa na mwaka 202.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. David Mathayo ameeleza kuwa katika Bajeti ya mwaka 2024/2025, Wizara ya Nishati imetekeleza vipaumbele vyake kwa kiwango cha kuridhisha ambapo Kamati hiyo imepongeza Viongozi Wakuu wa Wizara ya Nishati pamoja na Watendaji kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwa Kamati hiyo lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa Sekta ya Nishati inakuwa na mafanikio.

Kuhusu Bajeti ya Mwaka 2025/2026 Kamati imeishauri Wizara ya Nishati masuala mbali ikiwemo kuzidi kufuatilia upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya nishati, malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi,TANESCO kuongeza kasi ya ukarabati wa miundombinu ya umeme pamoja na kuendeleza miradi ikiwemo ya kusafirisha umeme ili wananchi wapate umeme wa uhakika.

# MRADI WA KUFUA UMEME WA JULIUS NYERERE WAKAMILIKA RASMI - DKT. BITEKO

- Asema ni ndoto ya watanzania kupata umeme wa uhakika
- Asisitiza kazi iliyobaki ni kuimarisha miundombinu ya kuwafikishia wananchi umeme
- Rais Samia na Rais wa Misri kuzindua rasmi Mradi wa Julius Nyerere



Mitambi 9 ya kufua umeme ya JNHPP

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewataka Watanzania kutegemea kupata umeme wa uhakika baada ya Mradi wa kufua umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere uliokuwa ukisubiriwa kwa shauku kubwa na Watanzania kukamilika rasmi.

Dkt. Biteko ameyasema hayo AprilI 5, 2025 baada ya kutembelea Mradi huo akiwa ameambatana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na uwekezaji, Mhe. Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. Hamadi Masauni pamoja na Viongozi wengine mbalimbali.

Amesema hivi sasa mitambo yote tisa imekamilika na inafanya kazi tayari, amefafanua kuwa kukamilika kwa Mradi huo kumechangiwa na maono ya Rais wa Awamu ya Sita, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye aliupokea Mradi ukiwa katika asilimia 33 ya utekelezaji wake na ndani ya kipindi cha miaka minne ya Uongozi wake ameweza kuukamilisha Mradi.

‘’Tumekuja leo tukiwa na furaha kubwa kwamba mitambo yote tisa imekamilika inazalisha umeme na nina furahi kuwajulisha Watanzania kuwa ile ndoto ya kuwa na umeme kutoka kwenye chanzo hiki kikubwa barani Afrika imekamilika, kazi iliyobaki ni kuimarisha miundombinu ya kuwafikishia watanzania umeme” Amesisitiza Dkt. Biteko

Dkt. Biteko amesema kutokana na nchi kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme kwa kiwango kikubwa sasa Serikali iko katika mchakato wa kukamilisha mazungumzo na nchi ya Zambia kwa ajili ya kuwauzia umeme na tayari njia ya umeme ya kuunganisha nchi hizo mbili inajengwa.

‘’Kile ambacho tumekua tukiongea miaka mingi kwamba Tanzania itakuwa na uwezo wa kuuza umeme nje ya nchi sasa imetimia katika kipindi hiki cha Serikali ya awamu ya sita baada ya msukumo mkubwa wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tuna mshukuru sana Mheshimiwa Rais”

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mhe. Profesa Kitila Mkumbo amesema kukamilika kwa Mradi huu ni ukombozi wa kiuchumi huku Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. Hamadi Masaun amesema Tanzania imeingia katika historia barani Afrika ambapo amesema kazi kubwa iliyobaki ni kutunza vyanzo vya maji ili kuulinda Mradi.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biiteko amelipongeza Shirika la umeme Tanzania TANESCO kwa usimamizi mzuri katika kutekeleza mradi huu kwa kiwango cha kimataifa na kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Mha. Gissima Nyamo-Hanga kwa jitihada zake katika kusimamia miradi mbalimbali ya umeme nchini.

Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere umegharimu zaidi ya Shilingi Trilioni 6.5 ambapo mpaka sasa serikali imeshalipa zaidi ya asilimia 99.5.

# DKT. BITEKO ASHIRIKI MKUTANO WA EAPP NCHINI UGANDA

- Tanzania yapongezwa kwa kuandaa Mkutano wa M300
- WB, AFDB kuunga mkono EAPP
- Mawaziri wa Nishati Mashariki Mwa Afrika wakutana Uganda



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko(wa nne toka kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na mawaziri wanaoshughulikia sekta ya nishati wakati wa ufunguzi Mkutano wa 20 wa baraza la Mawaziri wa Eastern Africa Power Pool (EAPP) unaofanyika tarehe 17 Aprili 2025 Jijini Kampala, Nchini Uganda

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko Aprili 17, 2025 jijini Kampala nchini Uganda ameshiriki katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Nishati wa nchi Wanachama wa Umoja wa Soko la Pamoja la Kuuziana Umeme katika Ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EAPP) na Mkutano wa Wakuu wa Mashirika au Taasisi za Umeme za nchi wanachama.

Kando ya mkutano huo, mawaziri hao walijadiliana kuhusu biashara ya kuuziana umeme miongoni mwa nchi wanachama.

Awali akifungua mkutano huo, Waziri wa Nchi wa Nishati wa Uganda, Mhe. Sidronius Opolot Akaasai amesema kuwa lengo la EAPP iliyoanzishwa Aprili 24, 2005 ni kuwa na uwiano sawa wa raslimali ya nishati katika ukanda huo.

Amesema hadi sasa EAPP ina nchi wanachama 13 na idadi inatarajiwa kuongezeka, ambapo nchi hizo zina nishati inayozalishwa kupitia vyanzo mbalimbali mfano maji, jua na gesi. Aidha, mahitaji ya umeme ni makubwa kuliko umeme unaozalishwa kwa sasa ambao ni megawati 19,000 pekee.

“Baadhi ya nchi bado zina changamoto ya nishati ya umeme na hivyo kushindwa kusambaza umeme kwa asilimia 100. Tunahitaji kuipa EAPP uwezo wa kutupatia umeme kwa vile nchi nyingi tayari zimeunganisha mifumo ya



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba (Katikati) akishiriki Mkutano wa 20 wa Baraza la Mawaziri wa Eastern Africa Power Pool (EAPP) unaofanyika tarehe 17 Aprili 2025 Jijini Kampala, Nchini Uganda

kusambaza umeme, sasa tunahitaji kufanya kazi pamoja ya kutimiza lengo letu la kuuziana umeme na kutumia vizuri raslimali tulizo nazo," amesema Mhe. Akaasai.

Amebainisha kuwa kupitia mkutano huo, watazindua ofisi za Bodi Huru ya Udhibiti (Independent Reguratory Board- IRB) ya Ukanda wa Mashariki mwa Afrika wa Kuuziana Umeme ambayo tayari ina baadhi ya wafanyakazi ikiwa na lengo la kufanikisha masuala ya biashara ya kuuziana umeme kwa nchi wanachama.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB), Dkt. Kevin Kariuki ameipongeza Tanzania kupitia kwa Dkt. Biteko kwa kuandaa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika - Misheni 300 (M300) uliofanyika Januari 27-28, 2025 jijini Dar es salaam, kwa kuwa umeonesha dhamira ya dhati nchi ya kutumia raslimali zake kutatua changamoto ya nishati barani Afrika.

Naye, Mwakilishi wa Benki ya Dunia (WB), Dkt. Joseph Kapeka amesema WB itaendelea kuunga mkono jitihada za Marais wa Afrika kupitia M300 ambao unalenga kuongeza upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 Kusini mwa Jangwa la Sahara ifikapo mwaka 2030.

Mkutano huo wa EAPP umeanza Aprili 16 na kumalizika Aprili 17, 2025 ambapo ujumbe wa Tanzania umejumuisha Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki, Mhe. Dennis Londo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesm Mramba pamoja na maafisa waandamizi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).









Waziri wa Nishati wa Nchi ya Uganda Mhe. Sadronius Opolot Akaasai akizindua Mkutano wa 20 wa Baraza la Mawaziri wa Eastern Africa Power Pool (EAPP) unaofanyika tarehe 17 Aprili 2025 Jijini Kampala, Nchini Uganda

# SERIKALI INAENDELEA NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA UMEME



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga akizungumza wakati akijibu hoja Aprili 10, 2025 bungeni jijini Dodoma.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga amesema Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya kusambaza umeme ili kuondokana na changamoto ya kukatika kwa umeme nchini.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo Aprili 10, 2025 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la la Mbunge wa Handeni Mjini, Mhe. Reuben Kwagilwa aliyeuliza ni lini Serikali itaondoa changamoto ya kukatika kwa umeme wilayani Handeni.

"Changamoto ya kukatika umeme Wilayani Handeni inatokana na uchakavu na urefu wa miundombinu ya kusambaza umeme. Katika kukabiliana na changamoto hii Serikali kupitia TANESCO inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya umeme ikiwa ni pamoja na kubadilisha nguzo za miti na kuweka za zege". Amesema Kapinga

Ameeleza kuwa, Serikali kupitia mradi wa gridi imara inaendelea na ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Mkata, Handeni ambacho kipo kwenye hatua za awali za ujenzi.

Ameongeza kuwa, ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Kilindi, Tanga umefikia asilimia 35 na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 kutoka Mkata kupitia Handeni hadi Kilindi umeffikia asilimia 30.

Akijibu swali la Mbunge wa Mlalo, Mhe. Rashid Shangazi aliyeuliza kuhusu Serikali kuona umuhimu wa kuharakisha ujenzi wa vituo vya umeme vya Mkata, Lushoto na Kilindi kutokana na umuhimu wa vituo hivyo kuimarisha upatikanaji wa umeme Mkoa wa Tanga, Mhe. Kapinga amesema tayari Wizara ya fedha imeihakikishia Wizara ya Nishati kuwalipa wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo kwa wakati ili waikamilishe.

Na kuhusu kusuasua kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkata hadi Kilindi kutokana na ulipwaji wa fidia, Mhe. Kapinga amesema fidia ya wananchi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkata, handeni hadi Kilindi ni takribani shilingi bilioni 2.63 ambayo Wizara ya fedha wameihakikishia Wizara ya Nishati kuilipa fidia hiyo.

Mhe. Kapinga ameongeza kuwa,

fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mkata, Handeni tayari wameshalipwa fidia.

Akijibu swali la Mbunge wa Hanang', Mhe. Mhandisi Samwel Xaday aliyeuliza ni lini Serikali itatatua changamoto ya kukatika kwa umeme Wilaya ya Hanang', Mhe. Kapinga amesema Wilaya ya Hanang' ipo katika mradi wa ujenzi wa gridi imara awamu ya pili ambapo kitajengwa kituo cha kupokea na kupoza umeme ambapo kwa sasa Serikali inaendelea na awamu ya kwanza ya mradi wa gridi imara.

Akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, Mhe. Grace Tendega kuhusu kukatika kwa umeme mkoani humo hasa Jimbo la Kalenga, Mhe. Kapinga amesema Serikali inayo mikakati ya kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Iringa ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya umeme kwa kubadilisha nguzo na nyaya chakavu.

Aidha, Mhe. Kapinga amesisitiza kuwa kutokea Mkoa wa Iringa, Tunduma hadi Katavi Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa kusafilisha umeme wa TAZA ambao unahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme ambavyo vitaboresha upatikanaji wa umeme maeneo yote ya ukanda huo na kuongeza kuwa mradi huo utaunganisha gridi za Taanzania na Zambia.

# KISHINDO CHA RAIS SAMIA MRADI WA JNHPP, ATIMIZA NDOTO YA MWALIMU NYERERE

- Mradi wa JNHPP wakamilika rasmi, watajwa kuikomboa Tanzania kiuchumi
- Dkt. Biteko awapongeza waandishi wa habari kuhabarisha umma mradi wa JNHP

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuwa kinara kufuatia jitihada zake za kukamilisha utekelezaji wa mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115.

Hayo yameelezwa Aprili 5, 2025 Rufiji mkoani Pwani na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko mara baada ya kutembelea mradi huo.

" Tunamshukuru sana Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha kutekeleza mradi huu ambao ulikuwa umefikia asilimia 30 wakati anaingia madarakani, kupitia uongozi wake aliweka mkakati mzuri uliosaidia kukamilisha mradi huu," amesema Dkt. Biteko.

Amesema kuwa mradi huo sasa umekamilika na una mitambo tisa itakayotumika kwa ajili ya kuzalisha umeme. Aidha, amewashukuru wakandarasi kutoka Kampuni ya Arab Contractors na wataalamu kutoka Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO) kwa kukamilisha mradi kwa weledi na viwango vizuri.

Amewahakikishiwa Watanzania kuwa Serikali inayoongozwa na Rais Samia ipo tayari kuhakikisha Watanzania wanapata umeme wa uhakika na inaendelea kujenga vyanzo vipya vya kuzalisha umeme nchini.

Amebainisha kuwa tayari Serikali imetoa shilingi trilioni 6.5 ikiwa ni gharama ya ukamilishaji wa mradi huo wa JNHPP.

Pamoja na hayo, Dkt. Biteko amevishukuru ma kuvipongeza vyombo vya habari nchini kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji na mafanikio ya miradi mbalimbali ya Serikali ikiwemo mradi wa JNHPP.

" Waandishi wa habari mliibeba ajenda hii ya Taifa, katika vyombo vyenu vya habari na kwa kweli vina mchango mkubwa.

Naomba mnifikishie shukrani zangu kwa wahariri na wakuu wa vyombo vyenu vya habari kwa kuhabarisha umma na kuna wakati hata kwa kutoa ufafanuzi wakati ambao tulihitaji wananchi wapate taarifa kamili na zenye usahihi," amesisitiza Dkt. Biteko.

Katika hatua nyingine, ameipongeza TANESCO na TECU kwa kukamilisha mradi kwa ufanisi.


Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Mhe. Prof. Kitila



Mkumbo amesema kukamilika kwa mradi huo ni ukombozi wa kiuchumi.

Naye, Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Hamadi Masauni amesema Tanzania imeingia katika historia barani Afrika ambapo amesema kazi kubwa iliyobaki ni kutunza vyanzo vya maji ili kuulinda mradi.

# DKT. BITEKO ASHIRIKI MKUTANO WA EAPP NCHINI UGANDA




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko(wa nne toka kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mawaziri wa Nishati wa nchi wanachama wa Umoja wa Soko la pamoja la Kuuziana Umeme katika ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EAPP) mara baada ya ufunguzi wa Mkutano wa 20 wa Baraza la Mawaziri wa Nishati wa nchi Wanachama wa Umoja wa Soko la Pamoja la Kuuziana Umeme katika Ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EAPP), mkutano huo umefanyika 17 Aprili 2025 Jijini Kampala, Nchini Uganda

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko Aprili 17, 2025 jijini Kampala nchini Uganda ameshiriki katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Nishati wa nchi Wanachama wa Umoja wa Soko la Pamoja la Kuuziana Umeme katika Ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EAPP) na Mkutano wa Wakuu wa Mashirika au Taasisi za Umeme za nchi wanachama.

Kando ya mkutano huo, mawaziri hao walijadiliana kuhusu biashara ya kuuziana umeme miongoni mwa nchi wanachama.

Awali akifungua mkutano huo, Waziri wa Nchi wa Nishati wa Uganda, Mhe. Sidronius Opolot Akaasai amesema kuwa lengo la EAPP iliyoanzishwa Aprili 24, 2005 ni kuwa na uwiano sawa wa raslimali ya nishati katika ukanda huo.

Amesema hadi sasa EAPP ina nchi wanachama 13 na idadi inatarajiwa kuongezeka, ambapo nchi hizo zina nishati inayozalishwa kupitia vyanzo mbalimbali mfano maji, jua na gesi. Aidha, mahitaji ya umeme ni makubwa kuliko umeme unaozalishwa kwa sasa ambao ni megawati 19,000 pekee.

"Baadhi ya nchi bado zina changamoto ya nishati ya umeme na hivyo kushindwa kusambaza umeme kwa asilimia 100. Tunahitaji kuipa EAPP uwezo wa kutupatia umeme kwa vile nchi nyingi tayari zimeunganisha mifumo ya kusambaza umeme, sasa tunahitaji kufanya kazi pamoja ya kutimiza lengo letu la kuuziana umeme na kutumia vizuri raslimali tulizo nazo," amesema Mhe. Akaasai.

Amebainisha kuwa kupitia mkutano huo, watazindua ofisi za Bodi Huru ya Udhibiti (Independent Reguratory Board-IRB) ya Ukanda wa Mashariki mwa Afrika wa Kuuziana Umeme ambayo tayari ina baadhi ya wafanyakazi ikiwa na lengo la kufanikisha masuala ya biashara ya kuuziana umeme kwa nchi wanachama.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB), Dkt. Kevin Kariuki ameipongeza Tanzania kupitia kwa Dkt. Biteko kwa kuandaa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika - Misheni 300 (M300) uliofanyika Januari 27-28, 2025 jijini Dar es salaam, kwa kuwa umeonesha dhamira ya dhati nchi ya kutumia raslimali zake kutatua changamoto ya nishati barani Afrika.

Naye, Mwakilishi wa Benki ya Dunia (WB), Dkt. Joseph Kapeka amesema WB itaendelea kuunga mkono jitihada za Marais wa Afrika kupitia M300 ambao unalenga kuongeza upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 Kusini mwa Jangwa la Sahara ifikapo mwaka 2030.

Mkutano huo wa EAPP umeanza Aprili 16 na kumalizika Aprili 17, 2025 ambapo ujumbe wa Tanzania umejumuisha Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki, Mhe. Dennis Londo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesm Mramba pamoja na maafisa waandamizi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

# MABALOZI KUTANGAZA UTALII WA TANZANIA KIMATAIFA

- Ziara ya utalii ya Mabalozi kuchochea ushirikiano wa Tanzania na mataifa mengine



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia Aprili 11, 2025 jijini Dar es salaam wakati wa uzinduzi na ufunguzi wa ziara ya Waheshimiwa Mabalozi katika vivutio vya utalii nchini.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuandaa ziara ya Mabalozi ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Zanzibar pamoja na mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Dkt. Biteko amesema hayo Aprili 11, 2025 jijini Dar es salaam wakati alipomwakilisha Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa katika uzinduzi na ufunguzi wa ziara ya Waheshimiwa Mabalozi ya katika vivutio vya utalii.

"Tanzania ni sehemu nzuri ya utalii duniani na ni imani yangu



Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Pindi Chana akizungumza Aprili 11, 2025 jijini Dar es salaam wakati wa uzinduzi na ufunguzi wa ziara ya Waheshimiwa Mabalozi katika vivutio vya utalii nchini

kuwa mtapata fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii ikiwemo Mlima Kilimanjaro ambao ni kivutio kikubwa duniani

kwa wapanda milima, lakini pia tuna hifadhi ya wanyama ya Serengeti, Ngorongoro na sehemu zingine," amesema Dkt. Biteko.

Ameongeza " Mtatembelea pia Mji Mkongwe Zanzibar na pia mtaweza kujifunza maneno machache ya lugha ya Kiswahili kupitia ziara hii. Tuna maziwa na mito mingi na maeneo mengine ya kihistoria kama Bagamoyo na vijiji vya wamasai,"

Pamoja ma hayo, Dkt. Dkt. Biteko amesema Mabalozi hao wanatakiwa kuendelea kukuza ushirikiano na baada ya ziara hiyo watakuwa mabalozi wazuri wa utalii wa Tanzania.

Naye, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Pindi Chana amesema leo ujumbe huo wa Mabalozi utatembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo Ngorongoro, Serengeti na Mlima Kilimanjaro.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Cosato Chumi amesema baada ya safari ya Arusha na Zanzibar, mabalozi wataendelea kuitangaza Tanzania kimataifa.

Balozi wa Comoro nchini na Kiongozi wa Balozi waliopo Tanzania, Mhe. Ahmada El Badaoui Mohammed Fakhi amesema kuwa kwa takribani miaka 11 aliyokuwepo nchini Tanzania hii ni mara ya kwanza kwa kuwa na tukio na namna hiyo.

"Kwa niaba ya Waheshimiwa Mabalozi wote niipongeze Serikali ya Tanzania kupitia Waziri wa Mambo ya Nje kwa kuandaa tukio hili," amesema Mhe. Fakhi.



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Cosato Chumi akizungumza Aprili 11, 2025 jijini Dar es salaam wakati wa uzinduzi na ufunguzi wa ziara ya Waheshimiwa Mabalozi katika vivutio vya utalii nchini



Balozi wa Comoro nchini na Kiongozi wa Balozi waliopo Tanzania, Mhe. Ahmada El Badaoui Mohammed Fakhi akizungumza Aprili 11, 2025 jijini Dar es salaam wakati wa uzinduzi na ufunguzi wa ziara ya Waheshimiwa Mabalozi katika vivutio vya utalii nchini.



Sehemu ya Waheshimiwa Mabalozi walioshiriki katika uzinduzi na ufunguzi wa ziara ya Waheshimiwa Mabalozi katika vivutio vya utalii nchini Aprili 11, 2025 jijini Dar es salaam

# KAPINGA ASEMA KIPAUMBELE CHA SERIKALI NI KUFIKISHA UMEME KWENYE TAASISI ZOTE



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga, akijubu hoja mbalimbali za wabunge tarehe 11 Aprili 2025, jijini Dodoma.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga amesema kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha Taasisi zote zinazotoa huduma za kijamii, kiuchumi na kidini zinafikiwa na nishati ya umeme wakati wa utekelezaji wa miradi ya umeme Vijijini.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo Aprili 11, 2025 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la la Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Maimuna Pathan aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itakamilisha kupeleka umeme kwenye Shule na Taasisi zote zikiwepo za dini katika Mkoa wa Lindi.

"Hadi kufikia mwezi Machi 2025, jumla ya Taasisi 1,272 zimeunganishiwa umeme katika Mkoa wa Lindi zikijumuisha: Zahanati 259; Vituo vya Afya 42; Hospitali 9; Shule za Msingi 554; Shule za Sekondari 151; na Taasisi za Dini 257 (Misikiti 142 na Makanisa 115). ". Amesema Mhe. Kapinga

Ameeleza kuwa, kupitia miradi inayoendelea kutekelezwa na kusimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Taasisi 27 zinatarajiwa kupatiwa umeme mkoani humo..

Akijibu swali la Mbunge wa Mbogwe, Mhe. Nicodemas Maganga aliyeuliza kuhusu Makanisa na Misikiti Mbogwe kutokuwa na umeme na mpango gani Serikali inao kuzipelekea Taasisi hizo umeme, Mhe. Kapinga amesema Taasisi hizo zitafikiwa na huduma ya umeme kupitia miradi ya Vitongoji inayoendelea katika Jimbo la Mbogwe,

Akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Dkt. Christina Mzava kwa niaba ya Mbunge wa Kishapu, Mhe. Boniphace Butondo aliyetaka kujua ni ipi kauli ya Serikali juu ya Kata ambazo hazijaunganishiwa umeme Kahama na Shinyanga, Mhe. Kapinga amesema Serikali ina mikakati ya kuweka miradi ya umeme pembezoni mwa miji ili wananchi waunganishiwe umeme kwa bei rahisi.

Awali, akijibu swali la msingi la Mbunge wa Kishapu, Mhe. Boniphace Butondo juu ya lini vijiji 42 vilivyobaki vya Wilaya ya Kishapu vitapatiwa umeme, Mhe. Kapinga amesema Jimbo la Kishapu lina jumla ya vijiji 117 ambapo hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2025 vijiji vyote 117 sawa na asilimia 100 vilikuwa vimekwisha unganishwa na huduma ya umeme kupitia miradi mbalimbali iliyotekelezwa na Serikali.

Akijibu swali la Mbunge wa Tarime Vijijini, Mhe. Mwita Waitara aliyetaka kufahamu wananchi wa Nywamwaga, Sirari na Nyamongo ni lini wataanza kuunganisha umeme kwa bei ya shilingi elfu 27, Mhe. Kapinga amesema maeneo ya Vijijini yanaunganishwa na umeme kwa shilingi elfu 27 na kwa yale ya pembezoni ipo miradi mingine ya pembezoni mwa mji.

# ONGEZEKO LA MAPATO NAMANGA LAMKOSHA DKT. BITEKO

- Ailekeza TANESCO kufunga Kituo cha Kupoza Umeme Longido
- Maelekezo ya Serikali yatekelezwa Longido
- Amuagiza Makonda kusimamia ufungaji vifaa vya maabara Sekondari ya Longido Samia




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia wananchi wa Kijiji cha Mundarara Wilaya ya Longido mkoani Arusha waliojitokeza kwenye mkutano wa hadhara Aprili 24, 2025 ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameeleza kufurahishwa kwake na ongezeko la ukusanyaji wa mapato katika kituo cha huduma za pamoja mpakani mwa Tanzania na Kenya cha Namanga.

Akizungumza Aprili 24, 2025 Namanga mkoani Arusha wakati katika ziara yake ya kutembelea miradi ya maendeleo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano Dkt. Biteko ameipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania Kituo cha Namanga kwa kufanya kazi kwa ufanisi.

" Nimefurahishwa sana na urahisi wa biashara na kila eneo limekuwa na ukuaji wa watu na bidhaa kwenye kusafirisha nje ya nchi ili kuleta fedha ya kigeni zitakazowezesha kufanya shughuli zingine nawapongeza sana, nawashukuru kwa kuwa na malengo makubwa ya kukusanya shilingi bilioni 124 na hadi kufikia leo mmekusanya shilingi bilioni 101 huku mkiwa na miezi kadhaa ya kuendelea kukusanya mapato" amesema Dkt. Biteko.

Amewataka watendaji hao kuendelea kuwa na utaratibu mzuri wa kurahisisha biashara kwa kuondosha mizigo inayosafirishwa kwa kutumia muda wa dakika 30 hadi 40 badala ya saa 2 kama ilivyokuwa hapo awali.

Ameendelea kusema kuwa Kituo hicho cha Namanga kilichofunguliwa mwaka 2018 na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, hayati Dkt. John Pombe Magufuli na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mhe. Uhuru Kenyatta kwa lengo la kurahisisha biashara kati ya nchi hizo mbili. Hivyo, watendaji hao waendelee kuwa mabalozi wazuri kwa kutangaza taswira njema ya Tanzania wakati wakitekeleza majukumu yao.


Awali akikagua Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia, Dkt. Biteko amesema kuwa baada ya siku kadhaa Kampuni ya Taifa Gesi itafunga miundo mbinu ya mfumo wa gesi shuleni ikiwa ni sehemu ya Serikali ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Pia, Dkt. Biteko amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. Paul Makonda kuhakikisha Shule hiyo inapata vifaa vya maabara ili wanafunzi waweze kujifunza kwa vitendo na si nadharia pekee.

" Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya hakikisheni hizi maabara zinafanya kazi kwa kupata vifaa, tabia ya wanafunzi kuchora bunsen bunner badala ya kuziiona na kuzitumia kwa kujifunzia kwa vitendo iishe, " amesema Dkt. Biteko.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akimwagilia mti aina ya Muembe (Mangifera Indica) mara baada ya kupanda Aprili 24, 2025 alipotembelea Shule ya Sekondari ya wasichana Longido Samia iliyopo Wilaya ya Longido mkoani Arusha ikiwa ni sehemu ya shamrashamra ya maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania.



Sehemu ya wananchi wa Kijiji cha Mundarara Wilaya ya Longido mkoani Arusha waliojitokeza kwenye mkutano wa hadhara Aprili 24, 2025 ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania.

Amebainisha kuwa amemuelekeza Mkuu huyo wa Mkoa kuangalia namna ya kuweka uzio na kupata gari kwa ajili ya shule hiyo, huku akiwataka wanafunzi kujifunza kwa bidii ili watimize ndoto zao na kuwa Shule hiyo ni kielelezo cha Mkoa wa Arusha.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara katika kijiji cha Mundarara, Dkt. Biteko amesema madini ni kichocheo kikubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kuwa Kijiji cha Mundarara kimekuwa na uzalishaji wa madini ya rubi na kuwa anafurahishwa kwa kuona sasa Watanzania wanaweza kufanya kazi za uchimbaji wa madini.

Kuhusu umeme, Dkt. Biteko amesema “Vijiji vyote 52 vina umeme, kuna vitongoji 176 na vitongoji vyenye umeme ni 112 pekee. Kuna maeneo ambayo yanahitaji nguzo 25 na nimemuelekeza Meneja wa TANESCO ndani ya wiki tatu nguzo ziwekwe na watu wapate umeme. Nimemuelekeza pia Meneja na bosi wake transforma ije hapa wiki ijayo ifungwe na watu wapate umeme,” amesema Dkt. Biteko.

Vilevile, Dkt. Biteko ameelekeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kujenga njia nne za kupeleka umeme Loliondo, Namanga, Mundarara na Kamwanga na baadae kujenga kituo cha kupokea, kupoza na kusafirisha umeme ili kusaidia wananchi kupata umeme na kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Pamoja na hayo, amesema kuwa Rais Samia amefanya kazi kubwa ya kuwaletea Watanzania maendeleo na kuwaasa wamuunge mkono. Aidha, ametoa wito kwa wananchi kushiriki katika Uchaguzi Mkuu kwa kuchagua viongozi watakao waletea maendeleo.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko amebainisha kuwa katika kusheherekea miaka 61 ya Muungano ni vyema kila Mtanzania ajiulize kwa nafasi yake, amefanya nini yeye binafsi, lakini pia amefanya kitu gani hasa cha



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwa kwenye picha ya pamoja na Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya wasichana Longido Samia Aprili 24, 2025 alipotembelea Shule hiyo iliyopo Wilaya ya Longido mkoani Arusha ikiwa ni sehemu ya shamrashamra ya maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akipokea zawadi ya ng'ombe kutoka kwa wafugaji wa Kijiji cha Mundarara Wilaya ya Longido mkoani Arusha alipofanya ziara Aprili 24, 2025 ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania.

kukumbukwa kwa watu wake wa karibu, kwa jamii inayomzunguka na pia kwa Taifa.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Wizara ya Madini na Mbunge wa Longido, Mhe. Dkt. Steven Kiruswa amesema kuwa Serikali inayoongozwa na Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan imeendelea kusaidia miradi ya maendeleo ambapo wachimbaji wadogo wilayani humo sasa wana umeme wa uhakika.

Ameendelea kusema Wilaya hiyo imenufaika na miradi ya maendeleo ambapo usanifu wa barabara ya kutoka Siha hadi Longido unaendelea.

" Mgodi wa magadi soda wa Engaruka umetengewa fedha na tayari watu wako tayari kuja kuwekeza na itasaidia kujenga mji wa kisasa, tuna zaidi ya tani milioni 768 ambayo tunaweza kuchimba kwa muda mrefu bila kuisha. Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Samia wachimbaji wadogo wameweza kupata kiasi cha shilingi bilioni 9.999 ambapo Serikali inapata mapato, "amesema Dkt. Kiruswa.

Amesisitiza " Wilaya hii tumepewa fedha ya kujenga shule za sekondari sita katika kata zetu na tumebakiza kata tatu ambazo hazina shule za sekondari, kazi ya kujenga shule katika kata hizo inaendelea. Mafanikio haya yasingeweza bila kuwa na ushirikiano na mshikamano kati aya Chama Cha Mapinduzi, Serikali na viongozi wa kimila."

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. Paul Makonda amesema kuwa maelekezo ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa kuhusu ujenzi wa daraja, upatikanaji wa haki na kituo cha afya yamefanyiwa kazi.

" Tayari fedha zaidi ya shilingi milioni 250 imetolewa na baada ya wiki moja itaonekana kwenye mfumo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya. Kuhusu barabara, katika bajeti hii imetengwa fedha shilingi milioni 270, fedha hizi ni kwa ajili ya barabara ya Resingita yenye urefu wa km 13 na barabara ya Longido kwenda Meloe imetengewa shilingi milioni 105,"amesema Mhe. Makonda.

# MAWAKILI WASISITIZWA KUISHAURI SERIKALI KWA WELEDI

- Dkt. Biteko asema Serikali inatambua jitihada za Asasi za Kiraia kuhudumia Wananchi
- Rais Samia apongezwa kwa mageuzi katika huduma za sheria nchini
- Wawakili wahimizwa kuwa 'marafiki'wa Mungu badala ya Mahakama
- Dkt. Biteko ataja mikakati ya Serikali kuboresha huduma za sheria kwa wananchi



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Mawakili wa Serikali nchini, Aprili 15, 2025 jijini Dodoma.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewataka Mawakili wa Serikali kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya kitaaluma na kuhakikisha haki inatendeka miongoni mwa wanajamii.

Dkt. Biteko amesema hayo Aprili 15, 2025 jijini Dodoma wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Mawakili wa Serikali nchini.

"Ombi langu kwenu Mawakili wa Serikali, fanyeni kazi yenu kwa kuzingatia taaluma yenu ya sheria na kutenda haki, ni wajibu wenu kushauri kwa haki na fanyeni kazi bila kuathiriwa na maslahi ya mnaowashauri wala kuogopa," amesema Dkt. Biteko

Amesisitiza kwa kuwataka mawakili kufanya kazi ya kuiwezesha Serikali kuwahudumia wananchi kwa kuzingatia misingi ya haki."Fanyeni kazi ya kutetea Serikali yenu, nendeni mkaishauri Serikali na wakati wote mkatende haki, ifanyeni haki kuwa rafiki yenu na anayetokea mbele yenu aone haki imetendeka hata watakaokuwa wamehukumiwa wakiri wanastahili hukumu waliyopewa,"

Halikadhalika Dkt. Biteko amewapongeza Mawakili wa Serikali pamoja na wadau mbalimbali kwa kuunda na kuendesha Kamati za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya pamoja na kuendesha Kliniki za

Ushauri wa Kisheria bila malipo katika mikoa mitatu ya Dodoma, Kilimanjaro na Mwanza.

Amesema kuwa Serikali inatambua jitihada zinazofanywa na Asasi za Kiraia, na binafsi katika kuwahudumia wananchi kupata huduma za sheria huku akitaja baadhi ya asasi na vyama hivyo kuwa ni pamoja na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS)Legal and Human Rights Centre (LHRC), Tanzania Legal Aid Providers (TANLAP), Legal Service Facility (LSF), Tanzania Human Rights Defenders Coalition (THRDC) pamoja na Watoa Huduma za Msaada wa kisheria kama UNDP na UN Women..

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko amemuelekeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushughulikia changamoto mbalimbali zinazokikabili Chama hicho cha Mawakili wa Serikali ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kupata eneo la kujenga Ofisi za Makuu ya Chama na Vivutio vya Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali katika mikoa ya Arusha na Dodoma

Kwa upande wake, Waziri wa Habari, Utamaduni. Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Palamagamba Kabudi amesema kuwa Rais Mhe. Dkt. Samia ameimarisha sekta ya sheria kwa kutekeleza masuala mbalimbali mfano kusaidia uwepo wa haki jinai na Kampeni ya Msaada wa Sheria ya Mama Samia.

Mhe. Kabudi amesema kuwa umuhimu wa mkutano huo wa Mawakili wa Serikali kuwa ni kuwapa fursa kukutana na kubadilishana uzoefu wa kitaaluma, maslahi yao pamoja na kufahamiana.

Amewapongeza waasisi wa Chama hicho kwa kujenga taswira nzuri huku akiwaasa viongozi wengine watakao fuata kuendeleza taswira hiyo na amewataka mawakili hao kuwa marafiki wa Mungu badala ya Mahakama kwa kutenda haki na kusema kweli wakati wa kutimiza majukumu yao.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza Johari amemshukuru Rais Samia kwa kuendelea kuwa mkezi wa chama hicho kwa miaka mitatu na kusema kuwa ni wajibu wao sasa kukilinda na kuhakikisha kinafikia malengo yaliyokusudiwa

Pia, amebainisha kuwa kupitia mkutano huo wameidhinisha Mpango Mkakati wa Chama hicho kitakachoufuata na kutekeleza katika kipindi cha miaka mitano.

"Tumetengeneza Mpango Mkakati tunaokwenda kuutekeleza kwa shauku kubwa pamoja na viongozi wapya watakao chaguliwa katika Uchaguzi unaofanyika leo," amesema Mhe. Johari.

Amesema hadi kufikia Aprili 9, 2025 idadi ya mawakili wa Serikali imefikia 3,760 kutoka 2,652 waliosajiliwa wakati wa kuanzishwa kwa Chama hicho.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji amewaomba Mawakili na Maafisa Sheria wa Serikali kufanya kazi kwa uadilifu na kuzingatia sheria ili kujenga jamii imara na kupunguza mizozo katika jamii.

Amesema taasisi za sheria ziendelee kushirikiana ili kusaidia wananchi na kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi za kuhudumia jamii na kuleta ustawi kwa mustakabali kwa maendeleo ya nchi.

Kwa upande wake, Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali, Amedeus Shayo amesema Chama kimefanikiwa kujenga mfumo wa kielektoniki wa kukusanya ada kwa wanachama pamoja na kuimarisha ushirikiano na taasisi zinazoshughilika na masuala ya sheria za ndani na nje ya nchi." Rais Samia ameendelea kuwa kielelezo kizuri cha haki kupitia Kampeni yake ya Msaada wa Kisheria na Mawakili wanashiriki kutoa huduma za sheria kwa wananchi.

Pia, agizo la Rais Samia la Mawakili kuwa walinzi wa uchumi wa nchi kwa kutumia kalamu limeweka msingi wa Chama hiki na umesaidia kuboresha sheria kadhaa mfano Sheria ya Uwekezaji," amesema Shayo.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mstaafu na Jaji wa Mahakama Kuu, Mhe. Dkt. Eliezer Feleshi amemshukuru Rais Mhe. Dkt. Samia kwa kuzindua Chama hicho mwaka 2022 na kusema " Chama hiki kama kilivyoanzishwa na malengo yake kitabaki kuwa Chama bora cha kitaaluma kwa sababu Serikali na mawakili walijipanga kuwa nacho na hili ni jeshi la kulinda uchumi wa nchi kwa sheria na kalamu,"

Mkutano huo uliohudhuriwa na Mawakili wa Serikali kutoka katika Wizara, Wakala na Taasisi za Serikali, Mashirika ya umma umeongozwa na Kauli mbiu " Utawala wa Sheria katika Utekelezaji wa Majukumu ya Serikaki ni Nguzo Muhimu katika Kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050"

# DKT. BITEKO AWATAKA WATANZANIA KUTOGAWANYIKA WAKATI WA UCHAGUZI MKUU

- Asema Serikali ya Rais Samia itahakikisha miradi ya maendeleo inagusa wananchi
- Aelezea upekee wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar
- Asema Rais Samia anasema na kutenda



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwasili katika Shule ya Sekondari Migungani iliyopo Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Dkt. Biteko ametembelea Shule hiyo Aprili 23, 2025 ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za kuadhimisha miaka 61 ya Muungano wa Tanzania.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewataka wananchi kutogawanywa kwa itikadi ya dini wala siasa wakati huu kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Ubunge na Udiwani kwa manufaa ya Taifa.

Dkt. Biteko amesema hayo Aprili 23, 2025 wilayani Monduli mkoani Arusha wakati akizungumza na wanannchi mara baada ya kuzindua mradi wa maji katika Kijiji cha Esilalei.

"Ninatamani kuona hatugawanyiki na mtu yoyote wala hatuwekwi kwenye makundi ya dini wala ukabila. Nataka niwaombe wananchi wa Monduli pendaneni na shirikianeni na uchaguzi utakapofika chaguaneni kwa haki," amesema Dkt. Biteko.

Amewataka wananchi wa Monduli kuutunza mradi huo wa maji wa Esilalei " Nawapongeza Wizara ya Maji na RUWASA kwa kusimamia mradi huu mzuri na wa uhakika, bila shaka mtaona itakapofika Desemba mwaka huu awamu ya pili ya mradi itakuwa imekamilika,"

Pia, Dkt. Biteko amesema kuwa Serikali inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inawapenda wananchi wa Monduli na inawapongeza kwa uchapakazi wao kwenye kilimo na ufugaji.

Aidha, amewataka wachape kazi na kuwa Rais Samia amefikisha mradi huo wa maji kwa kuwa anapenda pia mifugo yao istawi. vilevile, amesema kuwa Rais Samia amemtuma kuwahakikishia wananchi hao kuwa wafugaji nchini wanakuwa daraja la juu kama walivyo wananchi wengine.

Aidha, amesema wananchi hao wanachohitaji ni Serikali tu iwapatie nyenzo kama maji, umeme na barabara ili kufanikisha shughuli zao ambapo tayari Rais Samia ameapa kuwapatia nyenzo hizo.

Kuhusu umeme, Dkt. Biteko amesema kuwa vijiji vyote vya Wilaya ya Monduli vimepata



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia wananchi waliojitokeza kwenye mkutano wa shamrashamra za maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania uliofanyika leo Aprili 23, 2025 katika Kijiji cha Migungani Wilaya ya Monduli mkoani Arusha.



Sehemu ya wananchi waliojitokeza kwenye mkutano wa shamrashamra za maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania uliofanyika leo Aprili 23, 2025 katika Kijiji cha Migungani Wilaya ya Monduli mkoani Arusha.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwashukuru wananchi wa Kijiji cha Esilalei waliojitokeza kushuhudia mradi wa Maji Esilalei Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Dkt. Biteko ametembelea mradi huo Aprili 23, 2025 ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za kuadhimisha miaka 61 ya Muungano wa Tanzania.

umeme na katika vitongoji 236, vitongoji 72 vimepata umeme na vilivyosalia vitapata huduma hiyo mara baada ya Uchaguzi Mkuu.

Akijibu ombi la Mbunge wa Monduli, Mhe. Freddy Lowasa " Nguzo za umeme 20 alizoomba Mhe. Mbunge kuanzia Alhamisi hadi wiki inayokuja tutaanza kuona watu wa hapa wanapata umeme bila masharti yoyote, katika maisha tunapimwa kwa kazi si kwa maneno,"

Pamoja na hayo, Dkt. Biteko amezungumzia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kusema kuwa Muungano huo wa miaka

61 ni wa kipekee duniani kwa kuwa mataifa kadhaa yamejaribu kuungana lakini yameshindwa. Aidha, Tanzania imeendelea kubaki Taifa moja lenye amani.

Naibu Waziri wa Wizara ya Madini Dkt. Steven Kiruswa amefurahishwa kwa Wilaya hiyo kupata maji na kusema kuwa maji ni uhai, hivyo anamshukuru Rais Samia kwa kusaidia pia mifugo kupata maji.

Mbunge wa Monduli, Mhe. Freddy Lowasa amesema kuwa kazi aliyofanya Rais Samia wilayani humo ni kubwa kwa kuwa huduma ya maji ilikuwa changamoto kubwa kwao.

" Kwa miaka mingi maji yamekuwa kero kubwa katika Wilaya yetu kwa kupata mradi huu tunaomba umpelekee shukrani zetu Rais Samia," amesema Mhe. Lowassa.

Meneja wa Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini Wilaya ya Monduli, Mhandisi Naville Msaki amesema kuwa mradi huo ulisanifiwa mwaka 2021 utahudumia wananchi 8,867 na mifugo 24,000 hadi sasa umefikia asilimia 96 na hadi kukamilika kwake utagharimu shilingi bilioni 2.7.

# WANAWAKE WACHANGIA 35% YA PATO LA TAIFA

- Dkt. Biteko afungua Mkutano wa TAWiFA
- Dkt. Biteko awataka wanawake kuwekeza katika teknolojia kufikisha huduma vijijini
- Uwekezaji kwa wanawake si hisani ni kimkakati kwa maendeleo ya Taifa



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa mwaka wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWiFA) Aprili 14, 2025 jijini Dodoma

Wanawake nchini Tanzania wanatajwa kuchangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa. Takwimu zinaonesha kuwa, zaidi ya 35% uchumi wa Tanzania hutokana na jitihada, juhudi na jasho la wanawake. Ambapo katika sekta mbalimbali za uzalishaji mali asilimia 70 ya nguvu kazi ya kilimo ni wanawake hasa katika mazao ya chakula.

Mchango wa mwingine wa wanawake unajidhihirisha katika biashara, viwandani na katika huduma za kifedha kupitia utafiti uliofanywa na Chama cha Mabenki Tanzania (TBA) mwa ka 2022 umeonesha wanawake ni 47% ya wafanyakazi wote wa sekta ya fedha. Pia wanashika 10% ya nafasi za kufanya maamuzi. Vile vile, 18% wakiwa wajumbe katika bodi za wakurugenzi sawa na wastani wa wanawake wawili katika kila bodi.

Hayo yamebainishwa Aprili 14, 2025 jijini Dodoma na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko wakati aliposhiriki katika ufunguzi wa Mkutano wa mwaka wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWiFA).

Pamoja na mafaniko hayo, Dkt. Biteko ametaja changamoto zinawakabili wanawake katika sekta ya fedha kuwa ni uhaba wa upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu, elimu duni ya masuala ya kifedha na uchache wa nafasi za kushiriki katika maamuzi ya Sera za Fedha.

Akizungumzia namna tamaduni, mila na desturi zinavyoweza kuwa changamoto kwa wanawake, amewataka wanawake nchini kuzingatia misingi ya malezi kwa watoto wao kwa kuwapa nafasi sawa watoto wa kike na wa kiume ili suala la usawa wa kijinsia lisiwepo badala yake iwe uwezo wa mtu yeyote kufanya kazi.

“ Kwa kushirikiana na wadau wengine Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za makusudi ili kutatua changamoto zinazomkabili mwanamke na hivyo kuchochea maendeleo yake,” amesema Dkt. Biteko.

Amebainisha baadhi ya hatua hizo



Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha, Mhe. Hamad Chande akiwa katika ufunguzi wa Mkutano wa mwaka wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWiFA) Aprili 14, 2025 jijini Dodoma.

kuwa ni kuwaamini na kuwapa wanawake nafasi za juu za uongozi na hivyo kuwepo katika kufanya maamuzi, kufanya Mapitio na Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2000, kuandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Ulinzi



Rais wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWiFA), Fikira Ntomola akiwa katika ufunguzi wa Mkutano wa mwaka wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWiFA) Aprili 14, 2025 jijini Dodoma.



Sehemu ya wanawake walioshiriki katika ufunguzi wa Mkutano wa mwaka wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWiFA) Aprili 14, 2025 jijini Dodoma.

na Usalama wa Wanawake na Vijana Vyuoni uliozinduliwa mwaka 2023 na kutoa fursa nyingine mbalimbali za kifedha na kiuchumi kwa wanawake.

Amesisitiza "Naomba hapa nitoe rai kwenu kuwa, mkiwa mnaendelea kutekeleza majukumu yenu, msisahau kuhusu kuwekeza katika teknolojia. Maana Dunia ya sasa inazidi kwenda zaidi katika maisha ya kidigitali. Hii itasaidia kurahisisha biashara na kufikisha huduma kwa wepesi hususan katika maeneo ya vijijini,"

Fauka ya hayo, Dkt. Biteko amesema kupitia mijadala na maazimio yatakayotolewa katika kikao hicho, itapatikana mbinu mpya za kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta ya fedha na uchumi wa nchi kwa ujumla kupitia mabenki, kampuni za bima, masoko ya mitaji. Pamoja na mbinu na njia mbalimbali za fedha mtandao zinazotatua changamoto zinazomkabili mwanamke katika sekta ya fedha.

Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha, Mhe. Hamad Chande amewapongeza wanawake nchini kwa kuanzisha Chama hicho kinacholenga kusaidia wanawake kiuchumi.

Amewahakikishia " Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa kutunga sera na sheria za kiuchumi ili wanawake na makundi mbalimbali yaweze kuimarika kupitia taasisi na vyama kama hivi. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana nanyi ili kuimarisha TAWiFA ili kuhakikisha nafasi ya mwanamke inazidi kuwa juu katika jamii."

Rais wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWiFA), Fikira Ntomola amesema kuwa wanawake nchini wameendelea kujishughulisha ili kuhakikisha sekta ya fedha nchini inakuwa. Aidha, jamii inapaswa itambue uwekezaji kwa wanawake si hisani bali ni uwekezaji wa kimkakati kwa maendeleo ya Taifa.

" Tunaahidi kufikisha elimu ya fedha kwa wanawake katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuandaa mafunzo na warsha kwa lengo la kuongeza uwezo wa kusimamia masuala yao ya fedha na biashara," amesema Bi. Ntomola.

Ameongeza kuwa TAWiFA imedhamiria kuleta mabadiliko chanya kuhusu ushiriki wa wanawake katika sekta ya fedha, aidha wanaishukuru Serikali kwa kuendelea kuweka sera na sheria zinazochochea uchumi jumuishi na uwepo wa usawa wa kijinsia kiuchumi na kijamii.

"Tumekuwa tukiwajengea uwezo wanawake wa kuendesha biashara zao kiufanisi, kukuza biashara zao na kupanua wigo wao kuhusu sekta ya fedha," amebainisha Bi. Ntomola.

Amewaomba wadau mbalimbali nchini kufungua milango ya fursa kwa wanawake, na kuwa TAWiFA ipo tayari kushirikiana nao kwa ajili ya kutoa elimu ya fedha kwa umma, pamoja na tafiti za kuendeleza miradi ya kusaidia wanawake ili kujenga sekta ya fedha iliyo jumuishi.

Makamu wa Rais wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWIFA), Nangi Massawe amesema kuwa Chama hicho kinakutanisha wanawake katika sekta ya fedha ili kujenga sekta yenye usawa kwa manufaa ya Taifa.

TAWiFA ina jumla ya wanachama 204 na kimeendelea kuhakikisha wanawake wanashiriki katika sekta hiyo ili kuchochea maendeleo.

# DKT. BITEKO AFURAHISHWA NA UTATUZI CHANGAMOTO ZA ARDHI MONDULI

- Akagua miundombinu Shule ya Sekondari Migungani, awataka wanafunzi kutunza miundombinu
- Asema Serikali itajenga mradi mkubwa wa umeme Monduli

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewapongeza viongozi wa halmashauri ya Wilaya ya Monduli kwa jitihada zao za kutatua migogoro ya ardhi wilayani humo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali kwa viongozi kutatua changamoto za wananchi katika maeneo yao.

Dkt. Biteko ametoa pongezi hizo Aprili 23, 2025 wilayani Monduli, mkoani, wakati akihutubia wananchi mara baada ya kukagua miundombinu ya shule Mpya ya Sekondari ya Migungani iliyopo wilayani humo.

"Naomba kuwapongeza tena viongozi wa Wilaya ya Monduli kwa kuendelea kufanya kazi nzuri sana hapa wilayani kwa maslahi mapana ya wananchi wa Monduli. Nimejulishwa kuwa, mmefanya mengi mno ikiwemo utatuzi wa changamoto na migogoro ya ardhi hapa wilayani. Nimejulishwa kuwa sehemu kubwa ya changamoto hizi mmefanikiwa kuzitatua hongereni sana," amesema Dkt. Biteko.

Ameipongeza pia kamati ya kutatua kero za wananchi inayoongozwa na Mkuu wa Wilaya, ikiwa na wataalamu mbalimbali ambayo imejiwekea utaratibu wa kupokea kero kutoka kwa wananchi na kuzipatia ufumbuzi, ambapo ameitaka pia iratibu zoezi la kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya ardhi.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akipanda mti aina ya Muembe (Mangifera Indica) Aprili 23, 2025 alipotembelea Shule ya Sekondari Migungani iliyopo Wilaya ya Monduli mkoani Arusha ikiwa ni sehemu ya shamrashamra ya maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania.

Akiwa shuleni hapo, Dkt. Biteko amewapongeza wananchi kwa kujenga shule hiyo ya Sekondari Migungani ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 85 ya ujenzi huku Serikali ikichangia shilingi milioni 500.

"Sote tunafahamu kuwa, elimu ni msingi mkubwa wa maendeleo. Sisi wana Monduli tayari tunayo shule yetu hii ambayo imeshakamilika. Hii ni miongoni mwa shule zilizopo Wilayani hapa ambazo zitaendelea kutupatia elimu kwa vijana wetu," amesema Dkt. Biteko.

Ameongeza kuwa Shule hiyo itakuwa na uwezo wa kuchukua wananfunzi 400 na hivyo amewataka wanafunzi kutunza miundombinu na kujifunza kwa bidi ili wajiandae kuwa wazalendo na raia wema huku wakiwa na uwezo wa kutafuta majibu ya matatizo watakayokumbana nayo.

Aidha, Dkt. Biteko amezungumzia maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano kwa kuwataka Watanzania kuenzi muungano huo kwa kujenga Taifa moja kwa kushikamana na kufanyakazi kwa pamoja kwa kushirikiana.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Mhe. Festo Kiswaga amesema kuwa Wilaya hiyo ni tegemeo kwa Chama Cha Mapinduzi na wamekuwa wakishirikiana na wananchi katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo.

Pia, amesema Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo barabara, hospitali, shule na kuwa Wilaya hiyo ni kati ya wilaya zinazofanya vizuri katika elimu na huku akiumshukuru Rais Samia kwa kuwekeza katika elimu nchini.

# TPDC, ZPDC ZAENDELEA KUSHIRIKIANA UENDELEZAJI SEKTA YA GESI NCHINI



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga, akijibu hoja mbalimbali za wabunge tarehe 14 Aprili 2025, jijini Dodoma.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga amesema Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) mwezi Februari, 2022 liliingia makubaliano ya ushirikiano na Shirika la Maendeleo ya Petroli Zanzibari (ZPDC) ambapo kupitia ushirikiano huo masuala mbalimbali yamekuwa yakifanyika kuiendeleza Sekta ikiwemo kubadilishana ujuzi na utaalam.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo Aprili 14, 2025 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la la Mbunge wa Kwahani, Mhe. Khamis Yussuf Mussa Mkenge aliyeuliza ni lini Serikali itainufaisha Zanzibari katika matumizi ya Nishati ya Gesi ili iweze kutumika katika magari.

"Mheshimiwa Spika katika ushirikiano huu suala la kupeleka gesi Zanzibar ni mojawapo ya agenda kuu. Pande zote mbili bado zinaangalia namna bora ya kufikisha gesi asilia Zanzibari ili iweze kupatikana kwa bei nafuu kwa watumiaji.". Amesema Mhe. Kapinga

# RAIS SAMIA, DKT. BITEKO WAMLILIA NYAMO - HANGA

- Dkt. Biteko afungua Mkutano wa TAWiFA
- Dkt. Biteko awataka wanawake kuwekeza katika teknolojia kufikisha huduma vijijini
- Uwekezaji kwa wanawake si hisani ni kimkakati kwa maendeleo ya Taifa




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwasili katika Kijiji cha Migungani Wilaya ya Bunda mkoani Mara kwa ajili ya kushiriki Ibada ya Mazishi ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Mhandisi Boniface Gissima Nyamo-Hanga. Ibada hiyo inafanyika Aprili 16, 2025.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Mashaka amesema kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa pole kwa waombolezaji wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Mhandisi Gissima Nyamo - Hanga kilichotokea Aprili 13, 2025 Bunda mkoani Mara.

Pia ameahidi kuwa Serikali itahakikisha kazi nzuri alizokuwa anazifanya Mhandisi Nyamo- Hanga inaendelezwa ili kuhakikisha Watanzania wanapata umeme wa uhakika.

Dkt. Biteko amesema hayo Aprili 16, 2025 katika kijiji cha Migungani, Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara wakati akiongoza waombolezaji katika mazishi ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania, Mhandisi Gissima Nyamo - Hanga

“ Mhe. Dkt. Samia alimpenda sana kijana wake hata msiba ulipotokea alinipigia simu
na ameniagiza nisimamie vizuri msiba huu kwa vile amesema angependa kuona Gissima anazikwa kwa heshima,” amesema Dkt. Biteko.

Ameongeza “ Mhe Rais ameniambia Mhandisi ameondoka lakini kazi alizofanya zitaendelea na bila shaka atawaletea TANESCO mtu mzuri atakayeweza pia kuliongoza Shirika na Serikali itahakikisha mipango na malengo yote yanaendelezwa,”

Dkt. Biteko ameendelea kwa kuwaasa viongozi kuishi kwa kuwa baraka kwa wengine na sio kuwasababishia maumivu huku akisema wasiwe vitunguu kwa kuwatoa machozi wengine.

Amesema “ Kwa niaba ya Mhe. Rais Samia ndugu zangu waombolezaji na familia naomba mpokee salamu za pole na na sisi Wizara tutaenzi mchango wake kwa kuendeleza yale mazuri aliyoyafanya,”




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akisaini kitabu cha maombilezo katika Msiba wa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Mhandisi Boniface Gissima Nyamo-Hanga. Ibada hiyo inafanyika Aprili 16, 2025 katika Kijiji cha Migungani Wilaya ya Bunda mkoani Mara.

Dkt. Biteko amemuelezea Mhandisi Nyamo - Hanga kama kiongozi mtulivu na muadilifu na aliyewaunganisha pamoja wafanyazi wa TANESCO "Gisimma alikuwa mtu anayekuja mbele yako akiwa na majibu ya tatizo unalokusudia, hakuwa mtu wa kulalamika mara nyingine hata walipokosea watendaji aliowaongoza alikuwa tayari kupokea changamoto zao na kuahidi kuzifanyia kazi. Binafsi nilimpenda sana,"

Aidha, amesema baada ya kuwa na umeme wa kutosha nchini, Mhandisi huyo aliongoza majadiliano ya kuuziana umeme na nchi ya Zambia.

Vilevile, ameiomba familia ya Mhandisi Nyamo- Hanga kuishi kwa umoja na upendo miongoni mwao.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Mhe. Profesa Sospeter Mhongo akizungumza kwa niaba ya wabunge amesema kuwa Mhandisi Nyamo - Hanga alishirikiana na wenzake kupendekeza kuweka umeme kwa gharama ya shilingi 127,000/= badala ya shilingi 300,000/=.

Marehemu alikuwa na uwezo mkubwa na hivyo nchi imepoteza bingwa aliyeweza kusimamia usambazaji wa umeme kwa gharama nafuu.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Alfred Mtambi amesema kuwa wananchi wa Mkoa huo wamepata pigo kubwa. Aidha, ametoa pole kwa familia ya marehemu, TANESCO na Wizara ya Nishati.

" Nawaomba niwakumbushe watumiaji wa barabara kutumia barabara vizuri ili kuepusha ajali, natoa agizo kwa Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Mara la kuendesha operesheni ya kuhakikisha barabara zetu zinapitika vizuri," amesema Kanali Mtambi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema kuwa msiba huo umeigusa Wizara yake na katika kuenzi mazuri aliyoyafanya atahakikisha Wizara inaendelea kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana ili kusaidia Watanzania kutumia nishati hiyo kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kujiletea maendeleo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme Tanzania, Dkt. Rhimo Nyansaho ametoa pole kwa familia kwa kuondokewa na mzazi na pia amesema wamepata faraja kuona Watanzania wengi wamejotokeza kuaga mwili wa marehemu.

" Alijiongezea ujuzi wa kusoma kozi za sheria na biashara ili aweze kujiongezea uwezo wa kufanya maamuzi sahihi wakati wa kutekeleza majukumu yake," amesema Dkt. Nyansaho.

Akiendesha ibada ya mazishi ya mazishi ya marehemu Nyamo-Hanga, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Mkoa wa Mara, John Mwita Maguge amewataka wanafamilia kuwa na faraja na kujipa moyo kwa kuwa huo ni mpango wa Mungu.

" Niwaombe kuwa Mungu atawafuta machozi ili muendelee kushikamana. Mungu wetu wa mbinguni awe pamoja na famia hii, wakati huu ni wa kwaresma hivyo wote tutubu na tumwamini yesu," amesema

Ameongeza "Niwakumbushe Watanzania kuwa mwaka huu ni wa kuchagua Rais, wabunge na madiwani hivyo tuhakikishe tunatumia nafasi hii ya kuchagua viongozi waadilifu na waaminifu,"

# NAIBU KATIBU MKUU NISHATI AONGOZA MAZISHI YA MUHAJIRI HAULE MLANDIZI-PWANI



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Dkt. Khatibu Kazungu, akizungumza wakati wa Msiba wa aliyekuwa dereva wa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la umeme Tanzania, TANESCO, Muhajiri Haule Mlandizi Mkoani Pwani.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Dkt. Khatibu Kazungu ameongoza viongozi na wananchi mbalimbali waliojitokeza katika maziko ya aliyekua dereva wa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la umeme Tanzania, TANESCO, Muhajiri Haule Mlandizi Mkoani Pwani.

Marehemu Haule alifariki dunia pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo katika ajali ya gari iliyotokea Tarehe 13 Aprili,2025 Wilayani Bunda Mkoani Mara.

Naibu Katibu Mkuu huyo amemuelezea Marehemu Haule kuwa alikua mcheshi na mwenye upendo lakini pia kutokana na uwajibikaji wake alipewa dhamana ya kuwa dereva wa Wakurugenzi watendaji wa Shirika la TANESCO.

“Sisi kama Wizara tumepokea taarifa za msiba huu kwa huzuni kubwa sana, napenda kutumia nafasi hii kwa niaba ya viongozi wangu kutoa salamu za pole kwa familia ya Marehemu. Mhajiri alikua mtu mwenye upendo na mcheshi hivyo ni vyema kuyaenzi yale yote mazuri aliyofanya enzi za uhai wake” alifafanua Naibu Katibu Mkuu Kazungu.

Nao baadhi ya wakurugenzi wa TANESCO waliopita waliokufanya kazi na Marehemu akiwemo Dkt. Tito Mwinuka na Maharage Chande wamemuelezea Marehemu kuwa alikua mnyenyekevu na msikivu mwenye hofu ya Mungu.

Miongoni mwa Viongozi wa Taasisi waliohudhuria mazishi hayo ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya udhibiti wa huduma za nishati na maji EWURA James Andulile pamoja na chama cha wastaafu UWAWATA

Marehemu Muhajiri Haule alianza kazi TANESCO mwaka 1988 akilitumikia Shirika kwa kipindi cha miaka 37 lakini mwaka 2024 alistaafu kisha kuongezewa Mkataba maalumu.Marehemu Haule ameacha Mke ,Watoto wanne na mjukuu mmoja.

# RAIS SAMIA AIWEZESHA REA BILIONI 96.8 UTEKELEZAJI MIRADI YA UMEME VIJIJINI DODOMA - MHE. KAPINGA

- REA yaanza kwa kasi kufikisha umeme vitongojini
- Vijiji 580 Dodoma vyafikiwa na huduma ya umeme sawa na asilimia 100



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga akiwasha umeme katika moja ya nyumba ya ibada ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa mradi unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wa kusambaza umeme katika Vitongoji 15 (HEP IIA) katika Jimbo la Mvumi, mkoani Dodoma, Aprili 12, 2025.

**Na REA**

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imetoa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 96.8 ili kuhakikisha miradi ya umeme vijijini inatekelezwa katika mkoa wa Dodoma na wananchi wanapatiwa huduma ya umeme ili kuwapatia maendeleo ya kiuchumi na kijamii

Hayo yamebainishwa Aprili 12, 2025 na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga wakati wa uzinduzi wa mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji 15 (HEP IIA) katika jimbo la Mvumi mkoa wa Dodoma.

Mhe. Kapinga amesema, REA inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali pamoja na kuwasimamia kwa karibu wakandarasi wote waliopewa zabuni ya kutekeleza miradi ilikuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliopangwa ili iweze kuwanufaisha wananchi.

Naye, Mbunge wa Jimbo la Mvumi, Mhe. Livingstone Joseph Lusinde amesema Mwaka 2010 umeme ulikua kwenye vijiji viwili pekee lakini sasa vijiji vyote 60 vimefikiwa na huduma ya umeme na kuwaongezea chachu ya kufanya maendeleo wananchi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Mhe. Janeth Mayanja ameipongea REA kwa kuendelea kutekeleza miradi ya umeme vijijini ambayo imekuwa chachu ya maendeleo mkoani Dodoma.

Naye, Mkurugenzi wa Umeme Vijijini, Mha. Jones Olotu amesema kuwa, Mkoa wa Dodoma una jumla ya vijiji 580 ambapo vijiji vyote sawa na asilimia 100 vimepata huduma ya umeme kupitia miradi ya awali kama vile REA awamu ya kwanza (REA I), REA awamu ya pili (REA II), REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza (REA III Round I), na REA awamu ya tatu mzunguko wa pili (REA III Round II).

"Jumla ya vitongoji 1,773 na mitaa 225 vimefikiwa na huduma ya umeme kati ya vitongoji 3,212 na mitaa 258 ya mkoa wa Dodoma ikiwa ni sawa na asilimia 57 ya vitongoji vyote, " Amesema Mha. Olotu.

Mha.Olotu ameongeza kuwa, Wakala unaendelea na utekelezaji wa mradi wa HEP IIA katika vitongoji 150 vya mkoa wa Dodoma kupitia mkandarasi Derm Group Ltd ambapo hadi kufikia mwezi machi 2025, mkandarasi amekwisha kusimamisha nguzo katika vitongoji vyote.



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga akizungumza na wananchi wakati wa mkutano wa hadhara wa uzinduzi wa mradi unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wa kusambaza umeme katika Vitongoji 15 (HEP IIA) katika Jimbo la Mvumi, mkoani Dodoma, Aprili 12, 2025.

# REA YAPONGEZWA USAMBAZAJI WA UMEME VIJIJINI



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatib Kazungu akizungumza wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uliolenga kupitia bajeti na mpango kazi wa Wakala huo kwa mwaka 2025/26. Mkutano huo umefanyika Aprili 11, 2025 mkoani Singida.

**Na REA**

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego amuopengeza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kazi kubwa ya kufikisha umeme vijijini hali iliyobadili maisha ya wananchi vijijini.

Mhe. Dendego ametoa pongezi hizo Aprili 11, mkoani Singida wakati akifungua Mkutano wa Kwanza wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na REA uliolenga kupitia bajeti na mpango kazi wa Wakala huo kwa mwaka 2025/26.

“Nishati ya umeme ni nguzo kubwa kwa maendeleo ya Taifa lolote na watu wake. Nishati ya umeme vijijini ni msingi mkuu wa kuimarisha maendeleo ya haraka katika vijijini vyetu. Sote tumeshuhudia matokeo makubwa kwenye ukuaji wa uchumi, kuboresha maisha ya jamii zetu pamoja na kuchagiza utoaji wa huduma za kijamii.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imelipa swala la umeme vijijini kipaumbele cha kipekee na kuliweka katika mipango yake. Sekta ya Nishati, hasa nishati ya umeme vijijini kazi kubwa imefanyika. Tuwapongeze sana,” amesema Mkuu huyo wa Mkoa wa Singida.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatib Kazungu amewashukuru Wabia hao wa Maendeleo na kusema kuwa wamekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya nishati nchini huku akiwahakikishikia kuwa Serikali itaendelea kushirikiana nao kuhakikisha lengo la kuwafikishia nishati bora kwa bei nafuu wananchi wote



Mkurugenzi wa Umeme Vijijini, Mhandisi Jones Olotu akitoa taarifa wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uliolenga kupitia bajeti na mpango kazi wa Wakala huo kwa mwaka 2025/26. Mkutano huo umefanyika Aprili 11, 2025 mkoani Singida.




Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego akizungumza wakati wa kufungua Mkutano wa Kwanza wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uliolenga kupitia bajeti na mpango kazi wa Wakala huo kwa mwaka 2025/26. Mkutano huo umefanyika Aprili 11, 2025 mkoani Singida.




Mwenyekiti wa Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG), Kjetil Schie akizungumza wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Mwaka kati ya Wabia hao wa Maendeleo pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uliolenga kupitia bajeti na mpango kazi wa Wakala huo kwa mwaka 2025/26. Mkutano huo umefanyika Aprili 11, 2025 mkoani Singida.



Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Mhe. Balozi Meje Jenerali (mstaafu), Jacob Kingu akisisitiza jambo wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uliolenga kupitia bajeti na mpango kazi wa Wakala huo kwa mwaka 2025/26. Mkutano huo umefanyika leo Aprili 11, 2025 mkoani Singida.

linafikiwa.

Awali akizungumza, Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Mhe. Balozi Meje Jenerali (mstaafu), Jacob Kingu amesema kuwa, Tanzania imepiga hatua kubwa katika usambazaji wa umeme vijijini na mafanikio hayo yametokana na dhamira ya Serikali pamoja na mchango wa Wabia wa Maendeleo na kuahidi kuwa, REB itaendelea kuisimamia Mejimenti ya REA kuhakikisha miradi yote iliyopangwa inafanikiwa kwa wakati na katika ubora uliokusudiwa.

Naye Mwenyekiti wa Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG), Kjetil Schie ameipongeza REA kwa kazi kubwa ya kusambaza umeme vijijini na kuahidi kuwa wataendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha maisha ya wananchi kupitia sekta ya nishati.

"Tumeona ni kwa namna gani umeme unavyoweza kuboresha huduma za kijamii kama huduma za afya, upatikanaji wa maji na pia katika sekta ya elimu. Tulianza kushirikiana tukiwa na lengo la kutamani kuona kila Mtanzania akipata nishati ya umeme, na siku zinavyoenda tunaona lengo hilo linaenda kutumia. Tunapata matumaini sana na tunaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali kufikia lengo hilo," amesema Schie.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy, Mkurugenzi wa Umeme Vijijini, Mhandisi Jones Olotu amewashukuru na Wabia hao wa Maendeleo ambao ni Umoja wa Ulaya (EU), Benki ya Dunia, Serikali ya Norway, Serikali ya Sweden, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Benki ya Maendeleo ya Afrika na kuahidi kuwa REA itaendelea kutekeleza miradi kwa wakati na ubora uliopangwa ili dhamira ya Serikali pamoja na Wabia hao wa Maendeleo ya kuhakikisha kila mwananchi anapata nishati ya umeme inafikiwa

# REA KUSAMBAZA MITUNGI YA GESI ZAIDI YA 22,000 MKOA WA PWANI

- Kila wilaya kunufaika mitungi ya gesi 3,255



Afisa Maendeleo Mwandamizi kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Bi. Jaina Msuya (kushoto) akimkabidhi mtungi wa jiko la gesi wa kupikia Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Bw. Shangwe Twamala ikiwa ni ishara ya kuanza rasmi kwa zoezi la ugawaji wa mitungi hiyo ya gesi kwa wananchi ukiwa ni mkakati wa Serikali kupunguza matumizi ya nishati chafu za kupikia.

**Na REA**

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) umeitambulisha kampuni ya Manjis Gas ambayo imepewa jukumu la kusambaza mitungi ya gesi 22,785 itakayouzwa kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50 katika Mkoa wa Pwani.

Hayo yamebainishwa Aprili 16, 2025 katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoani Pwani na Afisa Maendeleo Mwandamizi kutoka REA, Bi. Jaina Msuya wakati wa uwasilishwaji wa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji mitungi ya gesi yenye ujazo wa kilo sita mkoani humo.

Msuya amesema kuwa mitungi ya gesi 22,785 itakayosambazwa mkoani Pwani ni utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia ambao una lengo la kuongeza matumizi ya nishati safi kufikia asilimia 80 ifikapo 2034.

"Lengo la mradi ni kuongeza upatikanaji wa huduma za nishati safi ya kupikia kwa kuwawezesha wananchi wengi kumudu gharama za bidhaa za nishati safi ili kutunza mazingira,kuokoa muda ili wananchi na jamii kwa ujumla kushiriki katika shughuli mbalimbali za kuiuchumi,kijamii ikiwemo siasa nakupunguza maradhi ya upumuaji na macho," Amesema Bi. Msuya.

Ameongeza kuwa gharama ya Mradi huo ni shilingi 398,737,500. Amezitaja wilaya zitakazonufaika kuwa ni pamoja na Wilaya ya Bagamoyo, Kibaha, Rufiji, Kibiti, Mkuranga, Kisarawe na Mafia. Kila wilaya itapata mitungi 3,255.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Bw. Shangwe Twamala ameipongeza REA kwa kuja na mradi huo na kuiomba iwe endelevu ili iweze kuwasambazia wananchi wengi nishati hiyo muhimu.

Naye, Mwakilishi kutoka kampuni ya Manjis gas, Bw. Gracious Maimu amesema watatekeleza mradi huo kwa kuzingatia makubaliano ya Mkataba wa kusambaza mitungi ya gesi ya kupikia pamoja na kutoa elimu na kuhamasisha wananchi ili wingi ili kuchochea matumizi ya nishati hiyo.